

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA IGUNGA (IGUNGA WSSA) KWA MWAKA 2020/21 – 2022/23

#### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-19-002

Mnamo tarehe 6 February 2020 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Igunga (Igunga WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi na usafi wa mazingira kwa mwaka 2020/21 hadi 2022/23. Majedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha bei na tozo za sasa na bei zinazopendekezwa.

#### Jedwali Na 1: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinayopendekezwa					
	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22	Mabadiliko	2022/23
Majumbani	1,060	70%	1,805.14	5%	1,895.39	5%	1,990.39
Taasisi	1,390	69%	2,344.50	13%	2,641.72	-2%	2,584.80
Biashara	1,750	53%	2,686.00	5%	2,821.06	5%	2,962.11
Viwanda	1,750	53%	2,686.00	5%	2,821.06	5%	2,962.11
Magati	1,500	7%	1,600.00	5%	1,680.00	5%	1,764.00
Wateja wa Jumla	3,460	7%	3,700.00	0%	3,700.00	8%	4,000.00

#### Jedwali Na 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho Mapya	Asilimia 20 ya Maunganisho Mapya		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				
Magati				

**Jedwali Na 3: Ada ya Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi/Marejesho)**

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2019/20	Mabad iliko	2020/21	Mabad iliko	2021/22	Mabad iliko	2022/23
Majumba ni	10,000	0%	10,000	50%	15,000	0%	15,000
Taasisi	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Biashara	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Viwanda	10,000	0%	10,000	150%	25,000	0%	25,000

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Igunga sababu kuu ya kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni kuiwezesha Mamlaka kukidhi ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo kutokana na mradi wa Ziwa Victoria. Bei na tozo zinazopendekezwa na Igunga WSSA zitaiwezesha Mamlaka kulipa gharama za uendeshaji, kuongeza mtandao wa huduma na kufanya uwekezaji katika miundimbinu ya maji na hivyo kuboresha huduma kwa wateja wake.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 26 Machi 2020** katika **Ukumbi wa Sakao** uliopo Igunga Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Igunga, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu **ifikapo tarehe 23 Machi 2020**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KATI, GHOROFA YA TANO, JENGO LA PSSSF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA IGUNGA**.

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**(EWURA)**  
**2 Machi 2020**